

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**

SHULE YA SEKONDARI MIRARE,
S.L.P 348,
RORYA.

15/12/2023

KUMB. NO. MMS/4168/F.1/15

MZAZI.MLEZI WA

S.L.P 250,
RORYA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIRARE 2024

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka **2024** katika shule ya sekondari Mirare, iliyopo umbali wa **KM 1.5** mashariki mwa Halmashauri Ya Wilaya Ya Rorya kijiji cha Ryagoro Kata Mirare. Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **08/1/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/1/2024** ndani ya siku kumi na nne (**14**), asipofika nafasi yake yaweza kuchukuliwa na mtu mwingine na kushindwa kufika kuripoti kwake shuleni bila taarifa yoyote ya msingi kwa tarehe tajwa hapo juu, hatua za kisheria na za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mzazi/ mlezi.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

3.0 SARE ZA SHULE

- Mashati mawili (**2**) aina ya tetron/cotton meupe yenye mikono mifupi yawe na kola na mifuko ya kushoto. (kwa wote)
- Tai rangi ya light blue na kaki (moja moja)
- Sweta (1) rangi ya blue kwa ajili ya baridi.(kwa wote)
- Suruali mbili zenye tanapu, moja kaki na nyingine light blue, epuka kushona au kununua suruali za piston na modal haziruhusiwi kabisa (kwa wavulana)
- Mkanda mweusi isiwe na kichwa kikubwa au mapambo mengine.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi (2) visiwe vya boot na kisigino kirefu na soksi jozi (2) nyeupe (kwa wote)
- Fika na bukta, t. shirt ya njano na kiatu cha raba (zitavaliwa kipindi cha michezo)
- T-shirt zinapatikana shuleni
- Sketi (2) aina ya tetron/cotton rangi ya light blue na kaki, weka mistari miwili mieupe kwenye sketi ya light blue na kaki, marinda yawe ya kati (si mdogo sana). Zote ziwe ndefu na zivuke goti (kwa wasichana).

Sare zote zitakaguliwa siku atakaporipoti mwanao, hivyo anapaswa kufika nazo zote zikiwa zimekamilika na zisiwe na kasoro yoyote.

Mahitaji mengine

- a. Daftari kubwa **09 counter book Q.2** kwa ajili ya notes za masomo yote.
- b. Daftari **ndogo 09** kwa ajili ya mazoezi ya darasani.
- c. Mathematical set 1
- d. **Dictionary** moja ya kiingereza kwa matumizi yake binafisi.
- e. Aje na miti mitano (5) ya misiligina kwa ajili ya kutunza mazingira
- f. Aje na **ream paper** aina ya **double A** moja (1) kwa ajili ya kufanyia mazoezi (mitihani) ya kila wiki na mwezi.

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

g. Aje na **file (faili)** moja kwa ajili ya kutunzia taarifa zake.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:-

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga/ kupigana
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kuoja/kuolewa
9. Kuapata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba.
11. Kudharau bendera Taifa.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama shuleni.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kutokuongea lugha ya kiingereza awapo shuleni.

NB. Mwanafunzi awapo shuleni au mtaani anapaswa kuheshimu sheria na taratibu za shule akiwa kama mwanafunzi.

KIAPPO CHA MWANAFUNZI NA MZAZI

Mimi ambaye nimechaguliwa kujiunga na masomo katika shule ya sekondari mirare mwaka huu, Ninakili kuwa nimesoma na kuelewa vyema sheria na kanuni za shule ninakubali kufuata sheria na kanuni hizo siku zote za uanafunzi wangu.

Mimi naahidi kumlea mwanangu kulingana na sheria na kanuni za shule, na mwanangu amekubali kufuata sheria na kanuni zote za shule. Pia naahidi kushirikiana na walimu kumlea mwanangu ili kuleta mabadiliko chanya katika elimu yake.

Hakikisha kuwa form ya afya imejazwa na kusainiwa na mganga wa hospital yoyote inayotambulika na kuirejesha shuleni siku atakaporipoti mwanao.

Simu namba 0763 169 277 – MKUU WA SHULE, 0686 431 496 – MAKAMU MKUU WA SHULE.

KARIBU SANA MIRARE SEKONDARI

.....
JOHN E. MATEKERE
MKUU WA SHULE